

TARATIBU ZA KUENDESHA USAILI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

1.0 UTANGULIZI:

Ujazaji wa nafasi za kazi katika ngazi mbali mbali katika utumishi wa umma utazingatia sifa, uwezo na utendaji mzuri wa kazi. Ujazaji huo utafanyika kwa njia ya ushindani wa wazi kwa kuendesha usaili au kwa uteuzi. Mamlaka za ajira katika utumishi wa umma zinapaswa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma wakati wa kuendesha usaili ili wale wenye sifa na uwezo waweze kuajiriwa.

2.0 USAILI

Kwa mujibu wa kanuni Na. 9-12 za utumishi wa umma za mwaka 2003 usaili katika Utumishi wa Umma utaendeshwa kama ifuatavyo:-

- 2.1 Usaili utafanywa kwa lugha ya kiswahili au kiingereza kulingana na mahitaji ya kazi. Kufuatana na mahitaji ya mwajiri, mtihani wa ziada unaweza kutolewa.
- 2.2 Wasailiwa wote watahojiwa na Bodi/Kamati Maalum ya Ajira yenye akidi (Quorum) isiyopungua nusu ya wajumbe.
- 2.3 Wasailiwa wote watahojiwa kwa kutumia maswali yanayofanana ambayo yanatakiwa yawe yameandaliwa kabla ya usaili. Maswali yatumungwe kufuatana na kazi iliyotangazwa.

- 2.4 Wasailiwa watatakiwa kuwasilisha picha mbili (passport size), vyeti vyao halisi (original certificates) ili vikaguliwe wakati wa usaili.
- 2.5 Utaratibu wa kutoa alama (marking scheme) utumiwe wakati wa usaili.
- 2.6 Jumla ya alama atakazopewa msailiwa zitapatikana kutokana na wastani wa alama za wajumbe walioshiriki katika kamati/Bodi ya ajira katika kumpima Msailiwa.
- 2.7 Wasailiwa watapangwa kufuatana na wastani wa alama walizopata kuanzia wa kwanza kwa kupata alama za juu hadi wa mwisho. Alama ya kufaulu ni asilimia 50 na kuendelea. Iwapo wasailiwa wawili wa jinsia moja watapata alama zinazolingana achukuliwe yule mwenye umri mkubwa zaidi.
- 2.8 Endapo wasailiwa wa jinsia tofauti watapata alama zinazolingana, msailiwa wa kike atachaguliwa.
- 2.9 Waajiri wawape kipaumbele walemavu kufuatana na Sheria ya Ajira kwa Walemavu Na.1 ya mwaka 1982.

3.0 HITIMISHO:

Kila mamlaka ya ajira katika utumishi wa umma inapaswa kufuata taratibu za kuendesha usaili ili kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika Utumishi wa Umma.

Ndugu msomaji, iwapo una maswali au maoni tafadhali wasiliana nasi kwa anwani ifuatayo:-

Katibu,

Ofisi ya Rais,

Tume ya Utumishi wa Umma.

Jengo la Accacia, Mtaa wa Samora,

S.L.P. 9143,

Dar es salaam.

Simu: +255(22)2126811/4, 216260, Fax +255(22)2114158